MASHIRIKA YANAYOONGOZWA NA WAKIMBIZI KATIKA AFRIKA MASHARIKI: MITAZAMO YA JAMII NCHINI TANZANIA

Uwezo Ramazani

Novemba 2022

Refugee-Led Research Series
Muhtasari

MUHTASARI

- Hamasa ya kufanya uchunguzi huu ni ushahidi unaojitokeza unaoonyesha kwamba mashirika yanayoongozwa na wakimbizi au kwa kifupi yakijulikana kama RLOs katika ukanda wa Afrika Mashariki yanatimiza wajibu mkubwa katika kukidhi mahitaji ya jamii. Kwa kuwa kabla ya uchunguzi huu hakukuwa na taarifa za kutosha kuhusu RLOs na utendaji wake nchini Tanzania, matokeo ya uchunguzi huu yanakidhi hitaji la ufahamu kwa kuchunguza aina, mawanda, na kazi za RLOs nchini Tanzania, maoni ya jamii hiyo na wadau kuhusu matokeo ya kazi za RLOs, pamoja na hali zinazochochea utendaji wa RLOs na uwezo wake.
- Kuanzia mwanzo hadi mwisho, uchunguzi huu ulifanywa na mtu mwenye uzoefu wa kuhishi ukimbizini.
- Kabla ya kukusanya taarifa, mpango ulifanywa ili kufahamu RLOs zote zilizopo Dar es Salaam, Nyarugusu, Nduta na Katumba. Matokeo yaliyo katika ripoti hii yanategemea uchunguzi wa kina wa RLOs 15 ambayo yalipatikana kupitia mahojiano ya watu 16 muhimu (KIIs) ambao ni viongozi wa RLOs, wadau 4 muhimu ambao si wa RLOs, vikundi 30 maalum vya majadiliano vilivyoundwa na wanufaika na wanufaika watarajiwa wa huduma za mashirika hayo, na vikundi 15 vya majadiliano vilivyojumuisha mameneja, wafanyakazi, na wafanyakazi wakujitolea wa RLOs.
- Katika kambi ya Nyarugusu, RLOs zilizo nyingi ni makundi madogo ya wanavijiji (CBOs) ambayo hufanya kazi bila kusajiliwa. Kwa maoni ya jamii hiyo, ni RLOs mbili tu zinazoonekana kuwa kubwa kwa kuwa zina majengo ya kudumu, zina zaidi ya wafanyakazi wa kujitolea 10 wanaofanya kazi muda wote, na zinaendesha kazi zao kwa uhuru. Mashirika hayo ni IBIEN, iliyo na wafanyakazi wa kujitolea 30 wa muda wote, na Group MISA, iliyo na vituo vinne vya kudumu. Katika ripoti hii, RLOs ambazo hazina majengo ya kudumu na yaliyo na wafanyakazi wa kujitolea wasiozidi watano wanaofanya kazi muda wote yanayochukuliwa kuwa madogo. RLOs hizo zimeanzishwa ama na watu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo au na Warundi, na hasa zinalenga kuwafundisha watu Kiingereza. Huduma zingine zinajumuisha afya ya uzazi, ukarabati wa majengo, elimu ya uraia, kuwapa misaada mayatima na wajane, kutengeneza sabuni, kutengeneza vitu kwa shanga na ushonaji.

- RLOs katika jiji la Dar es Salaam ni ndogo pia. Waliokuwa wakimbizi kutoka Kongo husajili RLOs kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kwa kuhusisha jamii za wenyeji katika mchakato wa usajili. Shirika lingine lilisajiliwa na kutambuliwa na serikali kuwa shirika lililoanzishwa na wahamiaji na wageni kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo wanaoishi kihalali wakiwa na vibali vya uhamiaji. Vikundi vya mlengo wa utaifa (Jumuia ya wakongo waishio Tanzania na Jumuia ya Wamalawi waishio Tanzania) hujikita katika kuwatetea wale wanaoishi mjini bila vibali wapewe vibali hivyo. Mashirika mengine hujikita katika kuwawezesha walengwa wao kujitegemea.
- RLOs nyingi zilianzishwa kati ya 2015 na 2020, ingawa si zote. Huko Nyarugusu, kuanzishwa kwa mashirika hayo kulichochewa kwa kiasi fulani na wakimbizi ambao tayari wamepata hifadhi katika nchi nyingine ya tatu (Marekani, Australia na nchi za Ulaya). Kuhusu jinsia, uchunguzi huu ulibaini shirika moja tu linaloongozwa na mwanamke, ambalo lipo Nyarugusu. Mashirika mengine mawili yanaongozwa na wanaume wanaojaribu kuwahamasisha wanawake kushika nyazifa za uongozi katika mashirika hayo.
- Viongozi wengi wa RLOs ni wasomi (katika mashirika yaliyoojiwa, viongozi kumi wana shahada, wawili wana diploma na watatu wamehitimu elimu ya sekondari). Viongozi wote wa RLOs wana umri wa zaidi ya miaka 30.
- Huko Nyarugusu, RLOs hupata fedha zake kwa kutegemea michango ya wanachama, ada za kujiunga na kujiandikisha kuwa mwanachama, shughuli za uzalishaji mali, misaada kutoka wenzao wanaoishi nje ya nchi, wafadhili binafsi na misaada ya vitu kutoka mashirika ya kibinadamu yanayohudumia wakimbizi kambini hapo. Huko Dar es Salaam, RLOs zote hutegemea michango ya wanachama na ada za kujiunga kama chanzo kikuu cha mapato.
- Wakimbizi wamehamasika kuanzisha RLOs ili kukidhi haja ya huduma zinazotolewa, kujitegemea, kuwawezesha watu kufikia hadhi fulani ya kibinafsi, kutumia ustadi walioupata kwa kufanya kazi na mashirika ya kibinadamu au kujitengenezea ajira.
  Huko Nyarugusu, RLOs mbalimbali zilizopo na shughuli zake zinafahamika miongoni mwa watu katika jamii ya wakimbizi, mkuu wa kambi, na pia na mashirika ya kibinadamu yanayohudumia wakimbizi . Watu katika jamii ambao hawanufaiki moja kwa moja na RLOs hizo wanafahamu kuhusu utendaji wake lakini hawawezi kutaja majina ya RLOs hizo moja kwa moja.
- Jijini Dar es Salaam, watu wanaonufaika moja kwa moja na RLOs hizo ndio wenye ufahamu kuzihusu. Watu ambao hawanufaiki nazo hawaoni umuhimu wa RLOs katika uimarishaji wa maisha na usalama wa jamii yao, wakisema kwamba vikundi hivyo huwasaidia wanachama wao tu.
- Huko Nyarugusu, jamii inaona kuwa RLOs zinasaidia katika upande wa elimu, hasa mafunzo ya lugha ya Kiingereza. Kwa kuwa mfumo wa elimu kambini hufuata mtalaa wa Kongo (upande wa wakongo) unaotolewa katika Kifaransa, ustadi wa Kiingereza unawawezesha washiriki kupata elimu ya juu na nafasi nyingi zinazotolewa na mashirika ya kutoa misaada. Watu katika jamii pia wanasema kwamba mashirika ya kuweka pesa na kutoa mikopo yanawasaidia wanachama kuanzisha shughuli za uzalishaji mali zinazowaletea mapato ambayo yanawainua kiuchumi na kuwapa stadi mbalimbali.
- Bado utendaji wa RLOs haujaleta mabadiliko katika sera na/au utendaji wa mashirika ya

kutoa msaada.

- Uwezo wa utendaji wa RLOs unategemea mambo mengi, kama vile mitandao ya watu walio nje ya nchi, rasilimali watu/viongozi na sheria zilizopo. Kwa mfano, viongozi wa RLOs kambini hushirikiana na wakimbizi wenzao ambao tayari wamepata hifadhi nchi ya tatu ili kupata misaada ya kifedha kutoka kwao. Kwa upande mwingine, sera za serikali ambazo haziruhusu RLOs kusajiliwa hukwamisha juhudi zao za kutafuta ufadhili wa kifedha wanaoweza kupata na hivyo kudhibiti uwezo wao wa kupanua utendaji.
- RLOs hukabiliwa na changamoto nyingi kama vile kutokusajiliwa na uwepo wa rasililmali chache (kwa mfano, watu wenye ustadi, rasilimali za kifedha, nyenzo na vifaa). Hata hivyo, washirika wa maendeleo wanataka kuwepo na viongozi wenye sifa za uzoefu na elimu ili kuwe na usimamizi mzuri wa ufadhili.
- RLOs hudai kwamba wanahitaji usaidizi kutoka kwa taasisi itakayowawezesha kupata usajili, pesa za kupanua huduma zao, na kujengewa uwezo wa kusimamia fedha, kuandaa maandiko ya miradi na usimamizi wa miradi.

Mapendekezo

- Wafadhili wanapaswa kufikiria kufadhili kifedha RLOs ambazo bado hazijasajiliwa kwa kuweka masharti yanayoendana na mazingira yao, kutetea mabadiliko ya sera serikalini, na kuzipa RLOs nafasi ya kushiriki katika sekta ya misaada ya kibinadamu.
- Serikali ifikirie kuruhusu RLOs kusajiliwa kama mashirika madogo ya maeneo ya mijini au hata vijijini ya wakazi wa maeneo husika (CBOs) au kama mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na kuendelea kuwapa ardhi ya kujenga ofisi zao.
- Kamishna Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi anapaswa kutambua kazi za RLOs, kutekeleza sera zilizotengenezwa katika ngazi ya kanda na kutetea mabadiliko ya sera serikalini.
- Mashirika ya kutoa misaada yanapaswa kuhusisha RLOs katika kufanya maamuzi kupitia muungano wa ushishirika wenye usawa, kuzipa RLOs fedha za kuandaa mazingira yanayofaa ya kujenga uwezo wao wenyewe, kukuza mawazo ya wakimbizi, na kuwa na ushirikiano utakaowawezesha kujenga uwezo wa utendaji.
- RLOs zinapaswa kuanzisha mtandao wa RLOs ili kuratibu jitihada zao za kujitetea wapate usajili na kutambuliwa.